

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

---

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI  
NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA  
MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (FUNGU 34)  
KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO  
KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025*

**MEI, 2026**

# YALIYOMO

	Ukurasa
<b>ORODHA YA MAJEDWALI .....</b>	<b>ii</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>1.0. UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1. Maelezo ya Jumla.....	1
1.2. Msingi wa Taarifa .....	1
1.3. Muundo wa Taarifa.....	2
<b>SURA YA PILI .....</b>	<b>4</b>
<b>2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO .....</b>	<b>4</b>
2.1 Maelezo ya Jumla .....	4
2.2 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa .....	5
2.3 Matokeo ya Ukaguzi.....	5
2.3.1 Mradi wa Ujenzi Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Arusha.....	6
2.3.2 Mradi wa Ujenzi wa Uzio wa kudumu katika Viwanja vya Ubalazi wa Tanzania, Addis Ababa, Ethiopia (Na.63911) .....	7
2.4 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; .....	8
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>10</b>
<b>3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ...</b>	<b>10</b>
3.1 Maelezo ya Jumla .....	10
3.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati .....	11
3.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara .....	11
3.4 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli .....	15
3.5 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina .....	17
3.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara.....	20
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>23</b>
<b>4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 .....</b>	<b>23</b>
4.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti.....	23
4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato .....	23
4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi .....	25
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>27</b>
<b>5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI .....</b>	<b>27</b>
5.1 Maoni ya Kamati.....	27
5.2 Ushauri wa Kamati.....	29
<b>SURA YA SITA .....</b>	<b>33</b>
<b>6.0 HITIMISHO.....</b>	<b>33</b>
<b>Kiambatisho Na.01 .....</b>	<b>36</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

<b>Jedwali Na. 1:</b> Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli hadi kufikia Februari, 2026.....	16
<b>Jedwali Na. 2:</b> Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na zilizopokelewa kwa Mwaka wa Fedha 2025/206.....	19
<b>Jedwali Na. 3:</b> Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa mwaka 2025/2026 na mwaka 2026/2027 .....	26

## SURA YA KWANZA

### 1.0. UTANGULIZI

#### 1.1. *Maelezo ya Jumla*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2025/2026; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa Hoja.

#### 1.2. *Msingi wa Taarifa*

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje ambayo kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazosisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa kukutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 23 Machi, 2026; ili kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama inavyoelekeza Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge; kwa ajili ya kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

### **1.3. Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia kikamilifu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

- (i) Sehemu ya Kwanza; ni utangulizi ambao unaeleza kwa ujumla kuhusu msingi na muundo wa Taarifa.

- (ii) Sehemu ya Pili; ambayo inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge.
- (iii) Sehemu ya Tatu hadi ya Nne ambazo zinachambua utekelezaji wa mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kuchanganua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.
- (iv) Sehemu ya Tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi. Aidha, sehemu hii inahitimisha taarifa kwa shukurani na kubainisha msimamo wa jumla wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mgawanyo huo wa taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa fedha 2025/2026 na kulinganisha na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na hatimaye kuamua kuhusu hoja ya wizara hii.

## SURA YA PILI

### 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

#### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi iliyotengewa fedha katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Arusha na Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia, ambayo ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili kama ifuatavyo: -

- (a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika mwaka wa fedha 2025/2026; na
- (b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Aidha, lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia kikamlifu hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo na hivyo kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## **2.2 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa **shilingi 45,540,026,000.00/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni mwendelezo wa ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Arusha); ukamilishaji wa vyumba vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (Dar es Salaam); na ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoanishwa awali Kamati ilitembelea miradi miwili ambayo ni; mwendelezo wa ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu unaotekelezwa mkoani Arusha ambao katika mwaka huu wa fedha ulitengewa **shilingi 34,000,000,000.00/=** na ujenzi wa uzio wa kudumu katika viwanja vya ubalozi wa Tanzania, Addis Ababa Ethiopia, ambayo ni sehemu ya mradi wa ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini uliotengewa **shilingi 10, 260, 000,000.00/=**.

## **2.3 Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako

Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo, hadi mwezi Machi, 2026.

### **2.3.1 Mradi wa Ujenzi Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Arusha**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa majengo sita (6) katika eneo la Lakilaki, Arusha na unatekelezwa na mkandarasi ambaye ni kampuni ya CRJE (East Africa) Limited, kwa thamani ya **shilingi 62,968,086,187.78** na mshauri mwelekezi, kampuni ya ARJ Built Environment consulting company (ABECC) kwa gharama ya **shilingi 2,956,000,000**.

Kamati ilipotembelea mradi huu ilielezwa kuwa muda wa utekelezaji ulipaswa kuwa miezi 18 tangu mkataba wa ujenzi uliposainiwa mwezi Agosti, 2023, hivyo ulipaswa kumalizika Februari, 2025. Hata hivyo, kutokana na mtiririko usioridhisha wa fedha za malipo kwa madai ya Mkandarasi, changamoto ya kubadilika kwa hali ya hewa, na upatikanaji wa vifaa vya ujenzi kutoka nje ya nchi mradi haukuweza kukamilika. Serikali imemuongezea mkandarasi mara mbili, hadi 27 Juni, 2025 na hadi Disemba, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati wa ukaguzi, mkandarasi alikuwa amelipwa kiasi cha **shilingi 24,887,384,392.84** ambacho ni sawa na takribani **asilimia 40** ya gharama za mradi. Aidha,

mshauri mwelekezi alikuwa amelipwa **shilingi 2,133,941,062.36** sawa na **asilimia ya 72** ya gharama ya ushauri elekezi, na utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 58**.

Kamati ilieleza kuridhishwa na utekelezaji wa mradi na kushauri Serikali iweke kipaumbele katika utengaji wa fedha ili kuwezesha mradi kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Takwimu zinaonesha hakuna uwiano mzuri kati ya upatikanaji wa fedha dhidi ya hatua ya utekelezaji, hali inayoashiria mkandarasi ametekeleza kwa hatua kubwa zaidi, lakini amelipwa kiasi kidogo.

### **2.3.2 Mradi wa Ujenzi wa Uzio wa kudumu katika Viwanja vya Ubalozi wa Tanzania, Addis Ababa, Ethiopia (Na.63911)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa uzio wa kudumu katika viwanja viwili vya Ubalozi wa Tanzania, vilivyopo eneo la Bole Kitema Woreda, Addis Ababa Ethiopia, ikiwa ni sehemu ya uendelezaji wa miliki za Serikali balozini. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ni **dola za Marekani 383,054.66**. Aidha, ujenzi wa mradi huu unaotekelezwa na kampuni ya Allure Construction PLC ya Addis Abba ulianza Mei, 2024 na kukamilika Septemba, 2025 na kukabidhiwa kwa Wizara mwezi Januari, 2026. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu, kiasi cha **dola za Marekani**

**226,776.62** sawa na **asilimia 59.2** ya gharama ya mradi kilikuwa kimelipwa kwa mkandarasi, na kiasi kilichosalia ambacho hati ya madai imewasilishwa hazina ni **dola za marekani 137,109.94**

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichosalia kiweze kutolewa na hazina ili kumlipa mkandarasi kwani ameishakamilisha na kukabidhi kazi. Aidha, hali hii inadhihirisha kuendelea kwa changamoto ya fedha za maendeleo kutopatikana kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu, kwani umeepusha athari za viwanja hivyo kutwaliwa na mamlaka za Jiji la Addis Ababa kama ilivyotokea awali, na kuendelea kuleta taswira nzuri ya taifa letu kimataifa. Hata hivyo, ni rai ya Kamati kwamba Serikali iharakishe mchakato wa kuanza ujenzi wa miundombinu ya majengo katika viwanja hivyo ili kuwezesha ubalozi kupata majengo ya ofisi na makazi na hivyo kuokoa fedha za Serikali zinazotumika kulipa kodi ya pango.

#### **2.4 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

- (i) Kwa kuzingatia hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na malipo yaliyofanyika kwa wakandarasi, utekelezaji wa miradi unaridhisha;
- (ii) Uwiano kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, ikilinganishwa na mtiririko halisi wa fedha kutoka Hazina ni mdogo. Mfano; mradi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu umefikia asilimia 58 ya utekelezaji, lakini fedha imepokelewa kwa asilimia 40 tu;
- (iii) Wakandarasi wanalazimika kusubiri kwa muda mrefu ili kupata malipo ya hati za madai kutokana na hatua za utekelezaji wa miradi. Mfano; katika mradi wa ujenzi wa uzio wa kudumu katika Viwanja vya Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia, mkandarasi amekamilisha na kukabidhi mradi tangu Januari, 2026 lakini bado anadai asilimia 40 ya gharama ya mradi; na
- (iv) Mtiririko wa fedha kutoka Hazina usioridhisha unaathiri muda wa utekelezaji wa miradi na kuongeza gharama za miradi husika. Mfano; mradi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ulipaswa kukamilika ndani ya miezi 18, lakini unatarajiwa kukamilika baada ya miezi 40 (Disemba, 2026).

## SURA YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

#### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ulilenga kulinganisha makusanyo ya maduhuli na lengo la makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa, hususan fedha za matumizi mengineyo na upatikanaji wa fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye Kamati kwa kipindi cha miezi ya Januari na Aprili, 2026 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu, na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Sehemu hii ya taarifa inahusu uchambuzi wa Kamati katika masuala yafuatayo:-

- (i) Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati;
- (ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli; na

(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.

### **3.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kuzingatwa na kufanyiwa kazi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa ya Mtoa Hoja ilieleza bayana namna ambavyo Serikali imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyodainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusesitiza kwamba, sehemu ya ushauri ambao haujatekelezwa kikamilifu inapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha ujao, 2026/2027.

### **3.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, ili kufuatilia ufanisi wa Wizara hii Kamati ilipokea Taarifa ambayo pamoja na mambo mengine inaonesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kuzingatia

vipaumbele mbalimbali. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni kuimarisha na kuratibu ushirikiano wa uwili, utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, na kuongeza ushawishi wa Tanzania katika masuala mtambuka kwenye jumuiya za kikanda na kimataifa. Taarifa hiyo imeonesha mafanikio makubwa yaliyozingatia maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio hayo yamechangiwa pia na hatua na nia thabiti ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa dhamira yake alipoingia madarakani alianza kwa kutoa mkono wa kheri (*olive branch*) kwa wanasiasa nchini, viongozi wa dini zote na asasi mbalimbali za kiraia. Hatua hiyo iliwavutia watu wa mataifa mbalimbali kushirikiana na vyama vya siasa, makundi ya dini na asasi za kiraia nchini kwa namna tofauti.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, msingi wa utayari huo upo pia kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977, Ibara ya 3(1) ambayo inaeleza kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya kidemokrasiana ya kijamaa, isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Aidha, Ibara ya 19 (1) ya Katiba inaeleza kuhusu stahili ya uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini au imani.

Sambamba na hilo, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuthamini uhuru wa dini zote kwa kuruhusu mashirika ya dini hizo kupata msamaha wa kodi, ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi Aprili, 2026 Serikali ilitoa msamaha wa kodi wa kiasi cha **Shilingi 7,461,049,255.00/=**. Hilo linatekelezwa kikamilifu ambapo hakuna dini yoyote iliyonyimwa msamaha wa kodi wala kuzuiwa kufanya shughuli za ibada yao.

**Mheshimiwa Spika**, aidha katika uhuru wa kuanzisha, kushiriki au kujiunga na jumuiya za jamii au vyama vya siasa, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuheshimu masharti ya Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezingatia hilo kwa kuruhusu wale wote waliokuwa nje ya nchi kwa hofu ya kukosekana kwa uhuru huo waweze kurudi nchini na alihakikisha wanarudi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa mikakati madhubuti ya Serikali ya kutengeneza uhusiano na mataifa mengine pamoja na taasisi za kidini zilizo nje ya nchi imewezesha kila dini iliyopo nchini kulindwa dhidi ya unyanyasaji na dhuluma ya ina yoyote kwa waumini wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa kwa kupitia Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, ambayo miongoni mwa misingi yake ni uhuru na mamlaka ya nchi (sovereignty) na kutofungamana na upande wowote (non – alignment), Wizara

hii itaendelea kueleweshwa jumuiya ya kimataifa hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha mshikamano na mtangamano nchini. Lengo ni kuweka mazingira sawa ya uhusiano na ushirikiano wa kimataifa kuwa na manufaa kwa taifa na washirika wetu. Miongoni mwa hatua hizo ni kuundwa kwa Tume Huru ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. Jukumu kubwa la tume hii lilikuwa ni kutafuta ukweli kuhusu matukio hayo na kutoa mapendekezo ya kuimarisha amani na maridhiano ya kitaifa. Aidha, katika muendelezo huo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda Tume ya Uchunguzi wa Kijinai wa matukio ya ghasia wakati na baada ya Uchaguzi wa 2025 kwa lengo la kuchunguza na kubaini wahusika wa vitendo vya kijinai na hatimae kupendekeza hatua za uwajibikaji. Watu wote waliotajwa kwenye Tume ya awali watahojiwa na kupewa fursa ya kujitetea.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za kudumisha misingi ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na utawala wa sheria katika kuhakikisha Taifa linaendelea kuwa na amani na utulivu. Sambamba na hilo, katika juhudi za kuendelea kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 -2030

katika Ibara ya 47(ii) inaielekeza Serikali kuhuisha na kukamilisha mchakato wa katiba mpya.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo ni rai ya Kamati kwamba, kwa kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya nchi yetu, ni vyema mataifa mengine yakatambua jitihada zinazochukuliwa na nchi yetu katika kukuza diplomasia na utawala bora. Aidha, mataifa hayo yanakaribishwa kwa lengo la kutoa mawazo na kufanya mjadala pale inapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo, kuliko kufanya maamuzi kwa kuegemea upande mmoja.

### **3.4 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,454,426,010.00/=** kutoka vyanzo mbalimbali Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania nje ya nchi. Kiwango hicho cha makadirio ni sawa na kilichowekwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia mwezi Februari, 2026 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa ni **Shilingi 1,094,309,000.00/=** sawa na **asilimia 75.24** ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho kilichokusanywa, **Shilingi 962,494,000.00/=** sawa na **asilimia 88** ya makusanyo yote ni

kutoka Balozi za Tanzania nje ya nchi, na **shilingi 131,815,000.00/=** sawa na **asilimia 12** ni kutoka Makao Makuu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa kiwango cha makusanyo kimeongezeka kwa **asilimia 33.4** ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **Shilingi 620,027,761.26/=** kilichokusanywa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025. vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila chanzo cha makusanyo na kubainisha mchanganuo huo kupitia jedwali kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 01**

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli hadi kufikia Februari, 2026**

<b>Chanzo</b>	<b>Makadirio 2025/2026</b>	<b>Makusanyo Februari,2026</b>	<b>% ya Makusanyo</b>
Makao Makuu	194,547,010	131,815,000.00	67.75
Balozi	1,259,879,000.00	962,494,000.00	76.40
<b>Jumla</b>	<b>1,454,426,010. 00</b>	<b>1,094,309,000.00</b>	<b>75.25</b>

*Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa makusanyo yaliyopatikana kwa kila chanzo hadi kufikia mwezi Februari, 2026 na kubaini yafuatayo: -

- (i) **Makusanyo kutoka Makao makuu ya Wizara;** hadi kufikia mwezi Februari, 2026 makusanyo yalikuwa **asilimia 67.75** wastani ambao ni mzuri kwani katika kipindi hicho ilikusudiwa makusanyo yawe angalau **asilimia 66;**

- (ii) **Makusanyo kutoka Balozini;** hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ilikusudiwa makusanyo yawe angalau **asilimia 66** ya lengo lililowekwa, lakini katika utekelezaji chanzo hicho kilikuwa kimekusanya kwa **asilimia 76.40** ya lengo la mwaka;
- (iii) Kwa ujumla makusanyo ya Fungu 34 – Wizara; yalikuwa ya kuridhisha kwani yalikuwa **asilimia 75.25** ambayo ni zaidi ya lengo tarajiwa la **asilimia 66**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa mwenendo wa makusanyo umeonesha matokeo ya kuridhisha katika vyanzo vyote kwani yalivuka lengo lililotarajiwa katika kipindi hicho. Hali hii inaakisi ama kuna usimamizi imara wa makusanyo, au kulikuwa na ukadiriaji wa chini ya lengo. Kamati inashauri Wizara ifanye tathmini na kuendelea kusimamia kikamilifu ili kuimarisha makusanyo kama makadirio ni halisi, au kuweka makadirio halisi kuhusu malengo ya kukusanya mapato iwapo makadirio hayakuwa halisi.

### **3.5 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa lengo la kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kufanya ulinganisho wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na kiasi kilichopokelewa kufikia mwezi Februari, 2026.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara iliidhinishwa na Bunge kiasi cha **Shilingi 340, 538,624,000.00/=** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi 294,998,588,000.00/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 45,540,026,000.00/=** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 237,555,659,297.25** sawa na **asilimia 67.76** ya fedha zote zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 219,350,522,801.94** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, kiwango ambacho ni sawa na **asilimia 80.15** ya kiasi kilichoidhinishwa kwa lengo hilo; **shilingi 13,674,294,852.05** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 64.09** ya kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya mishahara na **shilingi 4,530,841,643.26** ni kwa ajili ya maendeleo sawa na **asilimia 9.95** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Wizara ilikuwa imetumia kwa **asilimia 100** kiasi chote cha fedha kilichokuwa kimepokelewa katika kipindi hicho. Aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo ni ni chache, jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa miradi uliopangwa. Ni mtazamo wa Kamati kwamba mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha utaendelea kuathiri miradi iliyopangwa, hivyo


kipaumbele kinapaswa kuwekwa ili kuhakikisha fedha za maendeleo zinatolewa na Hazina kama ilivyo katika fedha za matumizi ya kawaida. Sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na ulinganisho wa fedha zilizopokelewa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Chati Na. 1**.

**Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na zilizopokelewa kwa Mwaka wa Fedha 2025/206**

<b>Mwaka</b>	<b>2025/2026</b>				<b>% +/-</b>
<b>Aina ya Matumizi</b>	<b>Kiasi Kilichotengwa</b>	<b>ASILIMIA</b>	<b>Kiasi Kilichopokelewa</b>	<b>Asilimia</b>	
<b>Mishahara (PE)</b>	21,337,111,000.00	6.3	13,674,294,852.05	64.09	5.76
<b>M/Mengineyo (OC)</b>	273,661,447,000.00	80.4	219,350,522,801.94	80.15	92.34.
<b>Maendeleo (DEV)</b>	45,540,026,000.00	13.3	4,530,841,643.26	9.95	2.9
<b>JUMLA</b>	<b>340,538,614,000.00</b>	<b>100</b>	<b>237,555,659,297.25</b>		<b>100</b>

*Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027na Usanifu wa Kamati*

## CHATI NA 1: Uwiano wa Fedha zilizopokelewa kwa Matumizi ya Wizara



*Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027 na Usanifu wa Kamati*

### 3.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuratibu masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa, kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli, kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki, kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, kukamilisha mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, Toleo la mwaka 2024 na mkakati wake,

kuratibu na kusimamia masuala ya wataanzania waishio ughaibuni, kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara, kusimamia na kuratibu masuala ya mikataba na makubaliano ya kimataifa; na kuratibu, kusimamia, kukuza biashara za kimataifa na kusimamia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichambua Taarifa za Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) na Kituo cha Mahusiano ya Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS – CFR) na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini (APRM).

Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa mtiririko usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina umeendelea kuathiri utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika kituo cha Dkt. Salim, na hivyo kuendelea kuchelewesha kufikiwa kwa malengo ya mradi huo.

Aidha, ukusanyaji wa mapato wa AICC ulikuwa kwa kiwango cha chini (asilimia 40), kutokana na baadhi ya mikutano ya kimataifa iliyokuwa imelipiwa kusitishwa na fedha kurudishwa kwa wateja, sambamba na kubomolewa kwa nyumba 211 ili kupisha ujenzi wa kituo kipywa na cha kisasa cha mikutano cha Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MKICC).

Awali nyumba hizo zilichangia katika mapato ya kituo kwa kupangishwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya uwepo wa changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni:-

- (i) Baadhi ya wadau ikiwemo sekta binafsi kutochangamkia ipasavyo fursa zitokanazo na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa;
- (ii) Baadhi ya nchini wanachama katika jumuiya za kikanda kutoheshimu baadhi ya mikataba na makubaliano ikiwemo kutolipa michango yao ya kibajeti kwa wakati, hatua inayoathiri uratibu na ushiriki wa nchi yetu katika utekelezaji wa program za mtangamano wa kikanda; na
- (iii) Kuzorota kwa hali ya amani na usalama katika baadhi ya nchi ndani na nje ya ukanda wa Afrika na hivyo kuathiri utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika**, ni mtazamo wa Kamati kwamba Wizara itaendelea kuzifanyia kazi changamoto hizo ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## SURA YA NNE

### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

#### 4.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa Taarifa kuwa, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vinne (4), idadi ambayo imepungua ikilinganishwa na vipaumbele vitano (5) katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuhusika na masuala ya kikanda pamoja na uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa; ni matumaini ya Kamati kwamba Wizara imejipanga ipasavyo kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi ili kufikia malengo na tija iliyokusudiwa na hivyo kuendelea kuimarisha utekelezaji wa dhana ya Diplomasia ya Uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano, mahusiano na ushirikiano wa Kimataifa kwa nchi yetu.

#### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia makadirio ya ukusanyaji wa mapato yanayopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, na kubaini kwamba Wizara imeweka lengo la kukusanya **Shilingi 1,511,000,000.00/=**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, **Shilingi 294,547,000.00/=** sawa na **asilimia 19.5** ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa na vyanzo vya Makao Makuu ya Wizara. Aidha, kiasi kinachobaki cha jumla ya **Shilingi 1,216,453,000.00/=** sawa na **asilimia 80.5** kinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Balozi za Tanzania nje ya nchi.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **shilingi 56,576,990.00/=** sawa na **asilimia 3.9** ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 1,454,426,010.00/=** kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa ni Balozi nne (4) tu za Tanzania nje ya nchi, katika majiji ya Lusaka - Zambia, Maputo - Msumbiji, Paris - Ufaransa, na Harare – Zimbabwe, ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la nyumba za Serikali. Balozi hizo kwa ujumla zinatarajiwa kuchangia **shilingi 512,931,785.00/=** sawa na **asilimia 42.12** ya mapato yote yaliyopangwa kukusanywa kutoka ofisi za balozi zilizo nje ya nchi. Aidha, kiasi hicho ni sawa na **asilimia 33.94** ya makusanyo yote yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa kiasi cha fedha kinachotozwa kama kodi ya pango kutokana

na upangishaji wa nyumba za Serikali zilizo nje ya nchi, ni kidogo sana ikilinganishwa na maeneo ambayo majengo hayo yapo katika nchi husika. Hii inachangiwa na majengo mengi kuchakaa kwani ni ya zamani na hayajakarabatiwa kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa kina ni matarajio ya Kamati kuwa lengo la makusanyo limezingatia uhalisia pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli, lakini Wizara itajitahidi kukabili changamoto hizo ili kuboresha ukusanyaji wa maduhuli katika mwaka wa fedha 2026/2027.

### **4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 359,326,404,000** kwa ajili ya matumizi yake. Kati ya fedha hizo **shilingi 312,961,378,000.00/=** sawa na **asilimia 80.79** ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 46,365,026,000.00/=** sawa na **asilimia 19.21** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Katika fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi 290,299,192,000.00/=** sawa na **asilimia 92.76** ya fedha yote

inayoombwa kuidhinishwa katika eneo hilo ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 22,662,186,000.00/=** sawa na **asilimia 7.24** ya fedha za matumizi ya kawaida ni kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa **shilingi 18,787,790,000.00/=** sawa na **asilimia 5.52** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa ni **shilingi 340,538,614,000.00/=**.

**Mheshimiwa Spika**, Sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na ulinganisho wake kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaonekana katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa mwaka 2025/2026 na mwaka 2026/2027**

MWAKA	2025/2026		2026/2027		% +/-
	AINA YA MATUMIZI	KIASI	ASILIMIA	KIASI	
<b>Mishahara (PE)</b>	21,337,111,000	6.3	22,662,186,000	6.3	6.2
<b>Mengineyo (OC)</b>	273,661,477,000	80.3	290,299,192,000	80.8	6.1
<b>Maendeleo</b>	45,540,026,000	13.4	46,365,026,000	12.9	1.8
<b>JUMLA</b>	340,538,614,000	<b>100</b>	<b>359,326,404,000</b>	<b>100</b>	

**Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027 na Usanifu wa Kamati**

## SURA YA TANO

### 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

#### 5.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi kama nilivyoieleza, Kamati ina mtazamo na maoni yanayojenga msingi wa ushauri utakaotolewa. Naomba kubainisha mtazamo na maoni hayo kama ifuatavyo: -

- (i) Upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa kiwango kidogo unaathiri malengo ya utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa. Mfano; hadi kufikia mwezi Machi, 2026 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 9.95** tu ya fedha za miradi ya maendeleo.
- (ii) Uwiano kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikilinganishwa na mtiririko halisi wa fedha kutoka Hazina ni mdogo. Mfano; mradi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu umefikia asilimia 58 ya utekelezaji, lakini fedha imepokelewa kwa asilimia 40 tu;
- (iii) Wakandarasi wanalazimika kusubiri kwa muda mrefu ili kupata malipo kulingana na hatua walizofikia katika utekelezaji wa miradi. Mfano; katika mradi wa ujenzi wa uzio wa kudumu katika Viwanja vya Ubalizi wa Tanzania, Addis Ababa, Ethiopia, mkandarasi

amekamilisha na kukabidhi mradi tangu Januari, 2026 lakini bado anadai **asilimia 40** ya gharama ya mradi;

- (iv) Mtiririko wa fedha za maendeleo kutoka Hazina usioridhisha unaathiri muda wa utekelezaji wa miradi na kuongeza gharama za miradi husika. Mfano; mradi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ulipaswa kukamilika ndani ya miezi 18, tangu ulipoanza Agosti, 2023, lakini sasa unatarajiwa kukamilika Disemba, 2026 (hii itakuwa ni baada ya miezi 40);
- (v) Kasi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim ni ndogo;
- (vi) Hatua ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Michuano ya Soka ya Mataifa Huru ya Afrika (AFCON) mwaka 2027, ikitumiwa vyema itachangia kuitangaza nchi yetu na kuinufaisha katika nyanja za utalii, michezo na uchumi kwa ujumla;
- (vii) Hatua ya Serikali kuboresho mfumo wa kielektroniki wa usajili wa diaspora kidijitali (Diaspora Digital Hub – DDH) inachangia kupatikana kwa takwimu sahihi za diaspora na hivyo kuchangia kuwezesha maamuzi sahihi ya kisera. Aidha, hatua hiyo itawajumuisha na kuwafanya wachangie kikamilifu katika ukuaji wa Uchumi wa taifa;

- (viii) Kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa kituo kipyaa na cha kisasa cha Mikutano cha Mlima Kilimanjaro (*Mt. Kilimanjaro International Convention Centre – MK ICC*) kutatoa fursa kwa nchi yetu kuwa na nguvu na uwezo wa kiushindani katika kuvutia na kuandaa mikutano ya kimataifa;
- (ix) Uelewa mdogo kwa wadau ikiwemo sekta binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa kunawafanya washindwe kutambua na kuchangamkia kikamilifu fursa zilizopo; na
- (x) Hatua ya baadhi ya nchi wanachama katika jumuiya za kikanda kutoheshimu mikataba na makubaliano ikiwemo kutolipa michango yao ya kibajeti kwa wakati kunaathiri uratibu na ushiriki wa nchi yetu katika utekelezaji wa program za mtangamano wa kikanda.

## **5.2 Ushauri wa Kamati**

- (i) Serikali itoe kipaumbele katika upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, ili kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa. Kamati imebaini kuwa mtiririko halisi wa fedha kutoka Hazina ni mdogo. Mfano; mradi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu umefikia asilimia 58 ya utekelezaji, lakini fedha imepokelewa kwa asilimia 40

tu. Aidha, SAS - CFR haikuwa imepokea kiasi chochote cha fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara;

- (ii) Serikali ihakikishe Wakandarasi hawalazimiki kusubiri kwa muda mrefu ili kupata malipo ya hati za madai kutokana na hatua za utekelezaji wa miradi, ili kutowakatisha tamaa na kuwaathiri kiuchumi. Mfano; katika mradi wa ujenzi wa uzio wa kudumu katika Viwanja vya Ubalizi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia, mkandarasi amekamilisha na kukabidhi mradi tangu Januari, 2026 lakini bado anadai asilimia 40 ya gharama ya mradi;
- (iii) Serikali ihakikishe kunakuwa na mtiririko mzuri wa fedha kutoka Hazina ili kutoathiri muda wa utekelezaji wa miradi na ongezeko la gharama za miradi husika. Mfano; mradi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ulipaswa kukamilika ndani ya miezi 18, lakini unatarajiwa kukamilika baada ya miezi 40 (Disemba, 2026);
- (iv) Serikali iweke kipaumbele katika kukabili changamoto zinazokwamisha kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, ili mradi huo ukamilike na kukiwezesha kituo

kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, kukamilika kwa mradi kutafanya kituo kuwa katika ubora unaoakisi hadhi kubwa na unguli wa kipekee wa Dkt. Salim Ahmed Salim, katika medani za kidiplomasia duniani;

- (v) Serikali iendelee kuboresha mfumo wa kielektroniki wa usajili wa diaspora kidijitali (Diaspora Digital Hub – DDH) ili kuongeza usajili na kupata takwimu sahihi za diaspora zitakazo iwezesha Serikali kufanya maamuzi yanayochochea ukuaji wa ushiriki wa diaspora katika ujenzi wa uchumi wa taifa;
- (vi) Serikali itoe kipaumbele katika kuhakikisha mradi wa kimkakati wa ujenzi wa kituo kipya na cha kisasa cha Mikutano cha Mlima Kilimanjaro (*Mt. Kilimanjaro International Convention Centre – MK ICC*) unatekelezwa na kukamilika kwa wakati ili kuwezesha nchi yetu kushindana kikamilifu katika kuvutia na kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa;
- (vii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wadau ikiwemo sekta ya umma na sekta binafsi kuhusu Diplomasia ya Uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na mahusiano ya kimataifa. Aidha, elimu hiyo iende sambamba na ushawishi wa wadau hao kuchangamkia na kunufaika na fursa zilizopo;

- (viii) Serikali iandae na kutekeleza kikamilifu mkakati kabambe utakaoiwezesha nchi yetu kunufaika katika nyanja za utalii, michezo na Uchumi kutokana na michuano ya Soka ya Mataifa Huru ya Afrika (AFCON) itakayofanyika Tanzania 2027;
- (ix) Serikali iendelee kutumia ushawishi wake kushirikiana na nchi nyingine wanachama na wadau mbalimbali ili kutafuta suluhu ya kudumu ya kuzorota kwa usalama kwa baadhi ya nchi wanachama wa jumuiya za kikanda, na kimataifa;
- (x) Serikali ya Tanzania iendelee kushawishi nchi wanachama kutekeleza wajibu wao wa kimkataba kulingana na masharti ya uanzishwaji wa jumuiya husika, ikiwemo kutoa michango ya kibajeti kikamilifu na kwa wakati. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe ili kushinikiza nchi hizo kutimiza wajibu wao ikiwemo kutoa michango; na
- (xi) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti iliyopita.

## SURA YA SITA

### 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao vimewezesha kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. Ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*): -

- |     |                                    |                |
|-----|------------------------------------|----------------|
| 1.  | Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb        | - Mwenyekiti   |
| 2.  | Mhe. Pascal Inyasi Chinyele, Mb    | - M/Mwenyekiti |
| 3.  | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb       | - Mjumbe       |
| 4.  | Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb         | - Mjumbe       |
| 5.  | Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb        | - Mjumbe       |
| 6.  | Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb         | - Mjumbe       |
| 7.  | Mhe. Zainab Rashi Kawawa, Mb       | - Mjumbe       |
| 8.  | Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mb  | - Mjumbe       |
| 9.  | Mhe. Christina Solomon Mndeme, Mb  | - Mjumbe       |
| 10. | Mhe. Fadhili Ally Liwaka, Mb       | - Mjumbe       |
| 11. | Mhe. Salum Khamis Haji, Mb         | - Mjumbe       |
| 12. | Mhe. Abdul Yussuf Maalim, Mb       | - Mjumbe       |
| 13. | Mhe. Ramadhan Muhidin Ramadhan, Mb | - Mjumbe       |

- |     |                                   |          |
|-----|-----------------------------------|----------|
| 14. | Mhe. Asya Ali Khamis, Mb          | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb     | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Zainab Abdallah Issa, Mb     | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Juma Omari Kipanga, Mb       | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Angela Charles Kizigha, Mb   | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Dkt. Lazaro KilliaKomba, Mb  | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia wasaa huu kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo (Mb), Manaibu Waziri Mhe. James Kinyasi Millya (Mb) na Mhe. Ng'waru Jumanne Maghembe (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Namshukuru Katibu Mkuu Balozi Dkt. Samwel Shelukindo pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushirikiano na mchango wao kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Idelphonice Leornad kwa kuwezesha utekelezaji mzuri wa shughuli za Kamati. Aidha,

naishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.



Najma Murtaza Giga, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO  
YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

26 Mei, 2026

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

- 1. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na binafsi iandae mpango mkakati unaotekelezeka ili kumaliza changamoto ya uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta ya umma na binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na mahusiano ya kimataifa. Kufanya hivyo, kutasaidia nchi yetu *kunufaika zaidi na fursa zitokanazo na mtangamano na uhusiano wa kimataifa.***

Wizara imeendelea na juhudi zake za kuimarisha upatikanaji wa habari kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na uhusiano wa kimataifa kupitia vyombo vya habari ikiwemo; televisheni, radio, magazeti, majarida, vipeperushi, maonesho, semina pamoja na mitandao ya kijamii ya X, Instagram, YouTube, Facebook, Blog na Tovuti. Aidha, Wizara inaendelea na utaratibu wa kutoa machapisho ya Jarida la Mambo ya Nje (*Foreign Affairs Bulletin*) linalotoka kwa kila robo mwaka ambayo yanatumika kutoa taarifa za shughuli za Wizara kwa wadau na umma.

Wizara inaendelea na maandalizi ya mkakati wa mawasiliano utakaohusisha wadau kutoka Serikalini na sekta binafsi ili kufikisha elimu na taarifa muhimu kwa ufasaha kwa wananchi kuhusu mtangamano wa kikanda na uhusiano wa kimataifa na hivyo kuwawezesha kunufaika zaidi na fursa mbalimbali ikiwemo ajira, biashara na uwekezaji na mafunzo.

**2. Katika kuhakikisha nchi yetu inanufaika katika nyanja za utalii na uchumi kwa jumla Serikali iandae mkakati maalum kwa ajili ya kutumika kufanya Public Diplomacy kwa nchi yetu kabla na wakati wa michuano ya Soka ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN-2025) na AFCON 2027 ambayo itafanyika Tanzania.**

Wizara kwa kushirikiana na sekta husika na kupitia Balozi za Tanzania Nje ya Nchi ilitumia majukwaa ya uwili, kikanda na kimataifa kutangaza fursa zinazopatikana nchini kupitia uenyaji wa Tanzania katika fainali za Mashindano ya CHAN yaliyofanyika mwezi Agosti 2025.

Wizara inaendelea na juhudi za kuitangaza nchi yetu ili kunufaika na fursa za uenyaji wa mashindano ya AFCON yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027. Fursa zilizopatikana ni pamoja na ajira kwa Watanzania katika miradi ya ujenzi wa viwanja vya mpira na miundombinu mbalimbali, kuongezeka kwa utalii, kuongezeka kwa biashara ya bidhaa za Tanzania, na kuongezeka kwa Pato la Taifa kupitia huduma za makazi na malazi.

**3. Wizara iandae mpango mahsusi unaotekelezeka kueleza mafanikio ya ziara za viongozi wa juu wanazofanya katika nchi mbalimbali duniani pamoja na za viongozi wengine wanaotembelea nchini. Kufanya hivyo, kutasaidia wananchi kufahamu faida na fursa zitokanazo na ziara za viongozi kwa nchi na kuweza kutumia fursa hizo kwa manufaa ya kiuchumi.**

Wizara imeweka utaratibu wa kutoa elimu na taarifa kwa umma

na wadau kabla ya ziara za Viongozi wa juu wa Kitaifa kufanyika kuhusu madhumuni/malengo na matarajio ya ziara husika. Aidha, Serikali kupitia Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu pia imeweka utaratibu wa kutoa mrejesho kwa umma na wadau kuhusu mafanikio yaliyopatikana kupitia ziara hizo za kimkakati ikiwemo Mikataba iliyosainiwa na fursa zilizopatikana ikiwemo; uwekezaji, ajira, ufadhili wa masomo, masoko, utalii na uchumi wa buluu.

kupitia mrejesho huo, Serikali pia hutoa maagizo kwa masuala yanayohitaji utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024. Orodha ya Mikataba na Hati zilizosainiwa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari 2026 zimeainishwa katika Kiambatisho Na. 1.

**4. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itumie ushawishi wake kushirikiana na nchi nyingine wanachama na wadau mbalimbali ili kutumia juhudi za kidiplomasia kwa kuzingatia mazingira yaliyopo kutafuta suluhu ya kudumu ya kuzorota kwa usalama kwa baadhi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya za Kikanda.**

Serikali imekuwa ikishiriki katika juhudi za Uwili, Kikanda na Kimataifa zinazolenga kurejesha hali ya amani na usalama katika Nchi Wanachama za Jumuiya za Kikanda zinazokumbwa na changamoto ya kuzorota kwa hali ya usalama na migogoro. Ushiriki huo unahusisha diplomasia, usuluhishi wa migogoro na kuchangia walinda amani ikiwemo Vikosi vya Kijeshi katika

misheni za ulinzi wa amani chini ya mwamvuli wa Jumuiya za Kikanda, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Juhudihudi hizi zinahusisha uratibu na uwenyeji wa Mkutano wa Ngazi wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kujadili suluhisho la hali ya usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hatua nyingine ni kuchangia walinda amani katika misheni za Kikanda ikiwemo; SADC nchini Msumbiji (SAMIM) na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (SAMIDRC).

**5. Serikali ya Tanzania iendeleze juhudi zake za kushawishi Nchi Wanachama kutekeleza ipasavyo masharti ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya, ikiwemo kutoa michango ya Jumuiya kwa wakati. Halikadhalika, Jumuiya ichukue hatua stahiki kwa mujibu wa mkataba kwa nchi zisizotoa michango ya Jumuiya.**

Tanzania ni Mwanachama hai na mwaminifu katika Jumuiya mbalimbali za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambapo imekuwa ikilipa michango yake ya uanachama kwa ukamilifu na kwa wakati. Aidha, Tanzania mara zote imekuwa ikizihimiza Nchi Wanachama ambazo zinadaiwa michango na zilizolimbikiza madeni kulipa michango hiyo kwa ukamilifu na kwa wakati. Aidha, pale inapobidi hupendekeza matumizi ya adhabu kwa mujibu wa Mikataba ya Uanzishwaji wa Jumuiya hizo.

**6. Wizara ianze mapema hatua za awali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuomba fedha kwa kuzingatia mpango wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi za ubalozi na majengo ya kitega uchumi inayotekelezwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi. Kufanya hivyo kutasaidia kufikiwa kwa tija iliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha hizo.**

Katika kutekeleza maelekezo ya Kamati, Serikali iliajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya tathmini na kushauri namna bora ya kuendeleza na kusimamia milki za Serikali nje ya nchi. Kufuatia ushauri wa Mshauri Elekezi, Wizara imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano wa Ukarabati na Uendelezaji wa Milki za Serikali Nje ya Nchi kuanzia Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 . Utekelezaji wa Mpango huo unashirikisha wadau wote muhimu katika Sekta ya umma na Sekta binafsi kuanzia ngazi ya maandalizi hadi utekelezaji wa miradi hiyo.

Utekelezaji wa Mpango huo unahusisha matumizi ya vyanzo mbadala vya fedha ikiwemo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi za Fedha kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Baadhi ya miradi inayotekelezwa kwa vyanzo mbadala vya fedha ni Ujenzi wa Majengo Pacha ya Vitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya na Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi Kinshasa kwa ubia na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Miradi mingine iliyo katika hatua za majadiliano baina ya Serikali

na Benki ya CRDB inajumuisha uendelezaji wa milki katika Balozi za Tanzania Lusaka, Zambia na Bujumbura, Burundi. Aidha, maandalizi ya hatua za awali zinajumuisha maandalizi ya nyaraka za mradi, usanifu, ununuzi wa wakandarasi kabla ya mradi kuanza kutekelezwa. Mathalan, Wizara imeanza maandalizi ya nyaraka na taratibu za awali kwa ajili ya miradi ya Abuja, Kinshasa na Addis Ababa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**7. Wizara iendeele kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025.**

Naomba kuihakikishia Kamati yako kuwa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kutekeleza kikamilifu maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo yamekuwa yakitolewa na yatakayoendelea kutolewa katika siku zijazo. Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa mara nyingine kwa michango yao ya kizalendo ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Asanteni sana!!!.